# Uanishaji wa Vigezo vya Utoaji wa Majina ya Utani kwa Walimu nchini Tanzania

*Davian Buguna* na *Salome Kotira*
*Taasisi ya Taaluma za Kiswahili, UDSM*

**Ikisiri**

**Wanafunzi huwapa walimu wao majina mbalimbali ya utani kipindi wawapo shuleni. Majina hayo hurejelea sifa tofauti tofauti zinazowahusu walimu hao ama moja kwa moja au si moja kwa moja. Je kuna sababu gani za utoaji wa majina hayo ya utani? Je ni vigezo gani hutumika katika kutoa majina hayo ya utani kwa walimu? Haya yalikuwa maswali yaliyohitaji kujibiwa na makala haya. Data za utafiti zimekusanywa kupitia hojaji zilizotumwa katika makundi 3 ya WhatsApp ya wanafunzi waliohitimu elimu ya sekondari katika shule ya Star, Nyasho,na Morogoro. Matokeo yanaonesha kuwa majina ya utani hutolewa kwa kuzingatia vigezo mbalimbali. Aidha, sababu zinazochochea utoaji wa majina hayo ni mahusiano mabaya kati ya walimu na wanafunzi, walimu kutofahamika majina kwa wanafunzi wao na tofauti za uzungumzaji.**

**Maneno Muhimu**: *Majina ya Utani, Walimu, Wanafunzi, Vigezo*

## Utangulizi

Majina ni utambulisho muhimu anaopewa mtu baada ya kuzaliwa na wazazi au watu wa karibu. Majina hayo huweza kutumika milele au kubadilishwa kwa sababu maalumu kama vile ndoa. Kusudi la utoaji majina huambatana na matarajio fulani kwa mhusika. Mutembei (2009) anathibitisha madai hayo kwa njia ya kuuliza swali kwamba kwa nini watu hutoa majina ya vitu, mahali, watu au matukio? Je, ni utambulisho au kielelezo cha yaliyopita au ni utabiri wa yatakayotokea? Akijijibu maswali hayo, Mutembei (ameshatajwa) anaeleza kuwa, kwa vyovyote vile kuna msukumo unaowafanya watu watoe majina. Majina tunayopewa huwa ni utambulisho wa asili zetu, kwa kumtambulisha mtu, eneo analotoka, tabia na sifa zake na humtofautisha mtu mmoja na mwingine.

Aidha, inasadikika kuwa majina haya huwa hayana uhusiano wa moja kwa moja na kirejelewa chake. Hivyo, Utofauti huo umekuwa kichocheo cha kuibuka kwa majina ya utani miongoni mwa wanajamii ili kuwapo na utambulisho halisi unaoendana na tabia na sifa zake ili kumtofautisha mtu mmoja na mwingine. Philips (1990) anaeleza kuwa majina ya utani ni seti ndogo ya majina au ni majina yasiyobainishwa wazi kwa mtu, na mara nyingi hayajulikani na watu wengi. Anadokeza kuwa majina hayo hayajulikani na watu wengi ni familia tu au watu wa karibu ndio ambao wanayatambua na kuyatumia. Naye, Starks na wenzake (2011) wanaeleza kuwa majina mengi ya utani wanayopewa watu katika maisha yao, huwa na nguvu ya kimatumizi kwa muhusika binafsi na utambulisho wake. Karibu majina mengi ya utani hubeba sifa za muhusika wa jina na kwa msingi huo jina hilo huibua dhana juu ya mhusika. Dhana hizo huchangia katika kuibua dhana zenye mielekeo mizuri au mibaya kwa mhusika wa jina la utani na mara nyingi huwa sio za kweli. Ni dhahiri kuwa majina ya utani huwa tofauti na majina halisi ya wahusika na malengo yake. Mehrabian na Pierce (1993) walieleza tofauti ya majina ya utani na majina halisi ya watu. Wanasema kuwa kila aina ya majina yana umuhimu katika nafasi yake. Mathalani, majina halisi ya watu yana hadhi zaidi katika mwelekeo wa kuchochea mafanikio, kujenga hamasa na fikra nzuri zaidi katika sehemu za kazi na ujuzi wa kitaalamu lakini majina ya utani hadhi yake inalenga zaidi juu ya kujenga umaarufu na kufurahisha.

Utamaduni wa utoaji wa majina ya utani hufanyika miongoni mwa jamii nyingi duniani kama tafiti mbalimbali zinavyodhihirisha (Chevalier, 2004, 2006; Wilson, 2008; Fernandez, 2008; Koss, 2006; Molefe, 2001; Wong, 2007). Tafiti nyingi zilijikita katika uchunguzi wa majina ya utani katika mitazamo wa kimofolojia kwa kuangalia njia za uundaji maneno zilizotumika katika uundaji wa majina hayo ya utani. Na tafiti chache zilijikita katika kueleza maana zilizofichwa katika majina ya utani kuhusu tabia za wahusika. Pia tafiti hizi zilishughulikia majina ya utani yaliyotolewa kwa vijana na wazee ndani ya jamii wa jinsia zote. Kimahususi tafiti zilizochunguza kuhusu majina ya utani nchini Tanzania kama vile (Mshihiri, 1970; Waziri na Dlourine, 1998; Suta na Mnyamba, 1999). Walichunguza utani katika muktadha wa makabila mbalimbali kama Wasambaa, Wapare, Wapemba

na Wabena. Tafiti hizi zimeonesha umuhimu wa utani katika kuwaunganisha wanajamii na kuleta utuluvu. Licha ya utofauti wa tamadini kama tulivyoeleza, taipolojia ya majina ya utani inadhihirisha kuwa yanatokea katika makundi mahususi (Crozier, 2002; Crozier and Dimmock, 1999; de Klerk and Bosch, 1996). Tafiti hizo tangulizi zinaelekea kuafikiana kuwa majina ya utani yanaelekea kudhihirisha sifa za kimaumbile za watumiaji kama vile uzito, urefu, rangi za nywele, tabia na haiba. Pia, majina mengine ya utani yanahusiana na historia ya mtu kama utamaduni, utaifa na vifupisho vya majina.

Makala haya yamechunguza majina ya utani wanayopewa walimu nchini Tanzania. Majina hayo hutolewa na wanafunzi kwa walimu wao katika mazingira ya shuleni. Eneo hili halijashughulikiwa kwa kiwango kikubwa hivyo kukosa maarifa ya kutosha juu ya mahusiano ya kiutani kati ya walimu na wanafunzi. Utamaduni wa mtanzania unaeleza utani kama jambo la furaha na linalounganisha watu katika jamii. Hata hivyo utani unachukuliwa kwa tahadhari kubwa hasa unapofanyika kwa watu wa rika na hadhi tofauti. Sengo (2009) anashadadia kuwa utani ni uhusiano wa kijamii uliojengeka baina ya pande mbili, wenye lengo la kufurahisha, kufunza, kukosoa na kukuza uhusiano kwa kuzingatia mila na desturi husika za jamii. Ni kielelezo kimoja wapo kinachotambulisha mila na desturi za watu katika jamii. Hata hivyo utani unatofautiana kwa namna moja au nyingine, kulingana na tamaduni na jadi za watu, kutoka jamii moja na nyingine. Aidha, uwapo wa tofauti za utani miongoni mwa jamii zimechochea kufanyika kwa utafiti huu ili kuweka bayana jinsi utani kati ya walimu na wanafunzi hasa katika kipengele cha majina unavyofanyika. Hivyo Makala haya yatabainisha vigezo vya utoji majina hayo ya utani na malengo ya utani huu miongoni mwa wanajamii hawa.

**Nadharia ya Simiotiki**

Nadharia ya simiotiki iliasisiwa na Fredinand Dessausure katika miaka ya 1970 anasema katika matumizi ya lugha, kuna vitu viwili kitaja na kitajwa. Anaeleza kuwa mara nyingi hakuna uhusiano wa moja kwa moja kati ya kitaja na kitajwa katika lugha. Hali ambayo husababisha kitu kimoja kuweza kuitwa majina tofauti kutoka jamii tofauti. Lengo la nadharia hii ya Simiotiki ni kutueleza juu ya matumizi ya lugha ya ishara na kile kinachorejelewa katika kazi ya fasihi. Nadharia hii inajishughulisha na ufumbuzi na ufumbuaji wa mafumbo katika kazi ya kifasihi. Nadharia hii ina misimbo mitano: Ambayo ni msimbo wa kimatukio, kihemetiki, kiurejelezi, iseme na kiutamaduni. Katika makala haya, mtafiti alitumia msimbo wa kiurejelezi. Msimbo huu hutumia maneno yenye kurejelea mambo mbalimbali yenye uhusiano fulani na maneno yenyewe. Hivyo, msimbo huu wa nadharia ya simiotiki ulimsaidia mtafiti kuainisha maneno mbalimbali yenye maana fiche yanayorejelea walimu mbalimbali nchini Tanzania.

**Methodolojia ya Utafiti**

Data za utafiti huu zimekusanywa kutoka kwa wanafunzi waliohitimu elimu ya sekondari nchini Tanzania katika shule ya Star mkoani Arusha, Nyasho mkoani Mara, na Morogoro mkoani Morogoro. Utafiti huu umetumia usampulishaji kusudio ili kupata watoataarifa. Usampulishaji kusudio ni aina ya usampulishaji ambayo mtafiti amechagua sampuli kulingana na malengo maalumu. Mtafiti alitumia mbinu hii kwa kusudi la kuwapata wanafunzi waliohitimu elimu ya sekondari na wanakundi la WhatsApp. Mtafiti alikusanya data kwa mbinu ya hojaji; maswali mawili yaliandaliwa kwa mfumo wa *google docs* yaliyowataka kutaja majina ya utani waliyokuwa wakiwaita walimu wao na maana za majina hayo. Swali la pili lilihitaji sababu za kutumia majina hayo. Hojaji hiyo ya kimtandao ilisambazwa kwa wanafunzi wahitimu wa sekondari kwa kutumia jamvi la WhatsApp, majamvi matatu ya wanafunzi waliohitimu yalitosheleza kutoa data iliyotakiwa. Mbinu ya hojaji iliteuliwa katika makala haya kwani mbinu hii humpa mtoataarifa uhuru wa kutoa taarifa kwa uhuru bila hofu. Data ya makala haya imechanganuliwa kwakutumia mkabala wa kitaamuli au maelezo. Data zilizokusanywa zilipangwa katika misimbo mbalimbali kwa kuzingatia ufanano wake na kisha zilitolewa ufafanuzi kwa kubainisha vigezo na sababu zilizotumika kutoa majina hayo ya utani.

**Uchambuzi wa Data na Mjadala wa Matokeo ya Utafiti**

Data za makala haya zimechambuliwa kwa kuzingatia malengo mawili, ambayo ni kuainisha vigezo vya utoaji majina ya utani na kufafanua sababu za utoaji wa majina ya utani. Hivyo, uchambuzi wa data ulifanyika kwa kuainisha kigezo, kutoa data kwa njia ya jedwali kisha ufafanuzi yakini ukafanyika.

**Vigezo vya Utoaji Majina ya Utani**

Majina ya utani yaliyobainika kupewa walimu yanadhihirisha kuwa hayatoki katika ombwe. Majina hayo hutokana na majina yanayotaja watu, mimea, mada za masomo, misemo, uradidi wa maneno, maumbile ya mwili na vifupisho vya majina halisi na matukio mengine ya kihistoria. Hivyo, data zinadhihirisha kuwa majina ya utani yaliyotolewa huwa ni tofauti lakini huweza kuanishiwa katika makundi yenye sifa sawa. Hivyo, makala haya yamejaribu kuanisha vigezo kadhaa ambavyo wanafunzi huvitumia wakati wa utoaji wa majina ya utani nchini Tanzania.

***Kigezo cha Maumbile ya Mwili***

Data za makala haya zinadhihirisha kuwa majina ya utani ya baadhi ya walimu yalitolewa kwa kuzingatia maumbile yao ya mwili. Wanafunzi ambao walihusika katika utoaji wa majina haya walitazama hali ya kimo, ulemavu, unene au wembamba, na viungo mbalimbali vya mwili na mwonekano wake. Mfano 1 unadhihirisha majina hayo.

**Mfano 1**

| Jina la Utani | Maana |
|---|---|
| Kisikio | Ulemavu wa sikio |
| Kakono | Ulemavu wa mkono |
| Vinyoya | Vinyweleo vingi |
| Mapua | Pua kubwa |
| Baunsa | Kifua kikubwa |
| Fuvu | Mwembamba |
| Moja | Mwembamba |
| Kipipa | Mfupi mnene |
| Kipotable | Mfupi mnene |

**Chanzo**: Data za Uwandani (2023)

Mfano 1 hapo umebainisha kuwa majina ambayo walimu hupewa na wanafunzi kama majina ya utani. Majina hayo yanadhihirisha sifa au hali ya maumbile waliyonayo walimu hao. Majina *kipotabo* na *kipipa* ni majina yanayotumika kumzungumzia mtu mfupi mnene, majina moja na fuvu hutumika kurejelea watu wembamba, majina kisikio na kakono hutumika kurejelea mtu mlemavu. *Mapua* hurejelea maumbile ya pua kuwa kubwa na *baunsa* hurejelea mtu mwenye mwili mkubwa hasa kifuani unaotokana na kufanya mazoezi. Sengo (2009) anauelezea utani kuwa ni uhusiano wa kijamii uliojengeka baina ya pande mbili, wenye lengo la kufurahisha, kufunza, kukosoa na kukuza uhusiano kwa kuzingatia mila na desturi husika za jamii. Hata hivyo utani unatofautiana kwa namna moja au nyingine, kulingana na tamaduni na jadi za watu, kutoka jamii moja na nyingine. Majina haya ya utani yaliyobainishwa hayadhihirishi sifa za utani zinazotajwa na sengo (keshatajwa) kwani yamebeba kejeli ndani yake. Vilevile mila na desturi za kitanzania hazitoi fursa ya watoto au vijana wadogo kuwatania watu wazima hasa kwa maumbile yao.

***Kigezo cha Vifupisho vya Majina***

Majina ya utani yaliyobainika kutolewa kwa kigezo hiki yanahusisha vifupisho vya majina ya walimu husika. Data zinaonesha majina mbalimbali ya utani waliyopewa walimu yanatofautiana kulingana na muundo wa majina yao. Mfano 2 unadhihirisha majina hayo ya ufupisho.

**Mfano 2**

| Jina la Utani | Maana |
|---|---|
| Diki | Dikteta |
| Kisu | Kisugage |
| Kiwi | Kiwiya |
| Simba | Mwakisimba |
| Para | Paralise |
| Dh | Double Happiness |

**Chanzo**: Data za Uwandani (2023)

Mfano wa pili unadhihirisha majina ya utani yaliyotokana na vifupisho vya majina halisi ya walimu mfano simba badala ya Mwakisimba, kisu badala ya Kisugage, kiwi badala ya Kiwiya. Aidha vifupisho vingine vya majina vilihusisha sifa alizonazo mwalimu husika. Mathalani, sifa zinazoendana na udikteta, wanafunzi walifupisha jina hilo na kumuita mwalimu diki. Pia, jina Para lilitokana na ugonjwa wa kuparalise aliokuwa nao mwalimu na DH lilitokana na mwalimu kupendelea kuvaa viatu vyenye jina la Dable Happiness hivyo wanafunzi walifupisha majina hayo. Kutokana na data hizi majina ya utani yaliyobainika yanatokana na vifupisho vya majina halisi ya watu, sifa na majina ya biashara.

***Kigezo cha Ufanano wa Wanyama***

Data za makala haya zinaonesha kuwa baadhi ya majina ya walimu yanatokana na ufananisho wa tabia au maumbile ya wanyama. Wanafunzi waliwafananisha walimu wao na wanyama wa porini na wakufugwa pia. Mfano wa 3 unadhihirisha majina hayo.

**Mfano 3**

| Jina la Utani | Maana |
|---|---|
| Faru | Hasira za haraka |
| Kenge | Sura isiyovutia |
| Beberu | Kutongoza wasichana sana |
| Beberu | Mbabe sana |
| Nguruwe | Mweupe sana |

**Chanzo**: Data za Uwandani (2023)

Majina ya utani katika mfano wa 3 yanadhihirisha kuwa maumbile na tabia walizonazo walimu zimechangia kupewa majina hayo. Majina faru na beberu yanadhihirisha tabia za walimu kuwa wakorofi na wenye hasira za haraka kiasi cha kuwapiga wanafunzi bila kuwa sikiliza. Aidha data zinaonesha majina kama kenge na nguruwe yalitolewa kwa walimu kwa kuangalia muonekano wao wa kimaumbile. Mwalimu aliyeitwa kenge alionekana kuwa na sura isiyovutia na aliyeitwa nguruwe alionekana kuwa na weupe wa ngozi. Aidha, ni kweli kuwa katika shule husika wapo walimu wenye sifa zilizotajwa lakini hawakupewa majina haya ya utani. Zipo sababu mahususi hasa zilizoukilia utolewaji wa majina hayo kama vile mwalimu husika kuwa na sifa au tabia husika iliyokithiri.

***Kigezo cha Ufanano na Watu Wengine***

Majina mengine ya utani waliyopewa walimu yalihusishwa na kufanana kwa baadhi ya sifa na watu wengine. Hivyo, wanafunzi waliwapatia walimu wao majina hayo ya watu wengine kwa kuwa tabia, maumbile yao yanafanana na wahusika hao. Mfano wa 4 unaweka bayana majina hayo ya utani na sifa zake.

**Mfano 4**

| Jina la Utani | Maana |
|---|---|
| Maximo | Kocha wa mpira |
| Mabala | Muhusika wa kitabu cha mabala the farmer |
| Gaucho | Mchezaji mpira |
| Yondo sister | Mwanamziki |
| Nyerere | Rais mstaafu wa Tanzania |
| Cyborg | Mwigizaji wa filamu |

**Chanzo**: Data za Uwandani (2023)

Majina yaliyotajwa katika mfano wa 4 ni majina ya watu halisi wanaojihusisha na kazi mbalimbali zilizotajwa hapo katika jedwali. Majina haya yalitolewa kama majina ya utani kwa walimu mbalimbali kwa sababu mbalimbali. Mathalani mwalimu aliyeitwa jina la Maximo alikuwa anahusishwa na michezo, walimu watatu wa shule tofauti waliitwa jina hili. Walimu hao walikuwa walimu wa michezo na makocha wa timu za shule hizo kama ilivyokuwa kwa Maximo mwenyewe aliyekuwa kocha mkuu wa timu ya taifa ya Tanzania. Pia, mwalimu aliyeitwa Yondo sister alikuwa mwalimu mwenye kusuka mtindo wa nywele na kuvaa kama mwanamziki huyo. Vilevile mwalimu aliyepewa jina la Cyborg alihusishwa na tabia ya ukatili na umbo lake kubwa alifananishwa na mcheza filamu huyo. Data za makala zinaonesha kuwa majina ya utani yanayotokana na majina halisi ya watu wengine, yanahusishwa na maumbile, kazi wanazopenda kufanya, haiba, na itikadi.

***Kigezo cha Mada za Masomo***

Makala haya yamebaini kupitia data kuwa majina mengine ya utani ya walimu hutokana na maneno yanayotaja majina ya wahusika wa vitabu, mada mbalimbali, au istilahi mbalimbali katika somo husika. Majina hayo walipewa walimu kama majina ya utani na wanafunzi wao kama yalivyobainishwa katika mfano wa 5.

**Mfano 5**

| **Jina la Utani** | **Maana** |
|---|---|
| Density | Mada ya fizikia |
| Mfecane | Mada ya historia |
| Assume the number | Mada ya hisabati |
| Monera | Mada ya baiolojia |
| Kishazi | Mada ya Kiswahili |
| Onkonko | Mhusika wa things fall apart |
| Cheaf Nanga | Muhusika wa things fall a part |
| Lawino | Muhusika katika song of lawino |

**Chanzo**: Data za Uwandani (2023)

Majina yaliyobainishwa katika mfano wa 5 yanadhihirisha kuwa yanatoka katika mada mbalimbali za kitaaluma. Wanafunzi waliwapatia walimu wao majina haya kwa sababu ya msisitizo wao wakati wa ufundishaji wa mada hizo. Walimu waliweka msisitizo zaidi kuzifundisha ili zieleweke kwa wanafunzi. Pia baadhi ya majina waliyatoa kwa walimu kwa sababu ya sifa za wahusika hasa wa vitabu vya fasihi zililandana na zile za walimu wao. Vilevile majina kama Monera na Onkonko yalitolewa kwa sababu ya namna walimu waliopewa majina hayo walivyokuwa wakiyatamka kwa namna ya kufurahisha. Hali iliyosababisha wanafunzi kuyatoa kama majina yao ya utani bila wao kufahamu.

***Kigezo cha Uradidi wa Maneno***

Majina mengine ya utani yalibainika kuwa yalitolewa kwa sababu ya mazoea ya walimu kupenda kurudia baadhi ya maneno wakati wa uzungumzaji. Data za makala haya zinaonesha maneno ambayo walimu hupenda kuyarudiarudia wakati wa uzungumzaji yalikuwa ya Kiingereza na Kiswahili. Mfano wa 6 udhihirisha maneno hayo yanayopendwa kusemwa na walimu wakati wa uzungumzaji.

**Mfano 6**

| **Jina la Utani** | **Maana** |
|---|---|
| Be flexible | Kaa tayari/ sawasawa |
| Father sio | Kurudia neno “sio” |
| Kilaza | Kuita wanafunzi kilaza “Mtu asiye na akili” |
| Ntakulima | Kuchapa fimbo |
| Nomale | Kurudia neno “normally” |
| Isn’t it | Kurudia neno “isn’t it” |

**Chanzo**: Data za Uwandani (2023)

Majina ya utani yaliyobainishwa katika mfano wa 6 yanadhihirisha kuwa walimu walipenda kuyatumia maneno hayo mara kwa mara. Maneno hayo yalitumika katika kueleza dhana iliyokatika hali ya mazoea kama vile neno normally, kusisitiza jambo neno kama sio, isn't it , kutahadharisha kama be flexible na ntakulima. Hivyo, matumizi ya maneno haya mara kwa mara yalisababisha kubadilishwa na kuwa majina ya utani ya kuwatambulisha walimu hao.

***Kigezo cha Muonekano wa Mavazi***

Majina mengine ya utani yalitokana na mwonekano wa nje wa walimu. Mwonekano unaozungumziwa hapa unahusisha aina ya mavazi walimu wanayovaa, namna wanavyoyavaa mavazi hayo na namna ya utembeaji wao. Data za makala haya zinadhihirisha majina mbalimbali yanayotokana na kigezo hiki kama ifuatavyo;

**Mfano 7**

| Jina la Utani | Maana |
|---|---|
| Mabwanga | Suruali pana |
| Mayeno | Kuvalia suruali tumboni |
| Tozi | Kuvaa t-shirt , jinzi na tai |
| Chek bob msoteo | Anatembea kwa kujikunja (kudunda) na huvaa raba |
| Kachumbari | Hajui kupangilia mavazi |

**Chanzo**: Data za Uwandani (2023)

Mfano wa 7 umeonesha majina ya utani mbalimbali ambayo walimu wamepewa na wanafunzi wao. Majina haya yanadhihirisha kuwa walimu hawa walidhirisha tabia au sifa fulani ambazo zilionekana wazi kwa watu wengine katika jamii. Data zinaonesha kuwa baadhi ya walimu walikuwa wakivaa aina fulani ya mavazi na jinsi ya uvaaji wao ulikuwa wa kipekee. Utofauti huo ndio ulichagiza utolewaji wa majina hayo kwa walimu husika.

**Sababu za Utoaji wa Majina ya Utani**

Data za makala haya zilibaini kuwa zipo sababu mbalimbali za utoaji wa majina ya utani kwa walimu. Wanafunzi wanaeleza sababu hizo kama vile mosi, kutofahamika kwa majina halisi ya walimu husika. Wanafunzi wanaeleza kuwa baadhi ya walimu hawawafahamu majina yao hivyo, majina ya utani hutumika kama njia rahisi ya kuwatambua. Wanafunzi huamua kutunga majina ya utani ambayo huendana na walimu husika ili kuwarahisisha mawasilianao yao kila siku wanapohitaji kuwarejelea. Majina haya ya utani mara nyingi hayafahamiki kwa walimu husika bali wanafunzi wenyewe.

Pia, mahusiano mabaya na wanafunzi yanachingia utoaji wa majina ya utani. Wanafunzi humpatia mwalimu jina la utani kwa kuzingatia mahusiano yao ya kila siku katika mazingira ya shule. Data zinadhihirisha kuwa ikiwa mwalimu anamahusiano mabaya na wanafunzi kama vile kuwapiga sana, kuwafukuza shule au tendo lingine lolote ambalo wanafunzi hulichukulia kama ni la kiunyanyasaji basi humpatia jina la utani lenye sifa mbaya. Mathalani walimu waliopewa majina ya faru, dikiteta, cyborg yalitokana na chuki ya wanafunzi juu ya tabia za walimu.

Aidha, kutambua upekee wa mwalimu katika Nyanja mbalimbali za maisha. Data zinadhihirisha kuwa majina mengine ya utani yalitolewa kwa sababu ya upekee alionao mwalimu husika. Mwalimu anaweza kutambuliwa kwa nafasi yake ya ufundishaji wa somo fulani, tabia na maumbile yake. Majina ya walimu ya utani ya walimu yanayotokana na maumbile ya mwili na mada sa masomo ni mifano halisi ya sababu hii.

Aidha licha ya sababu zote zilizobainishwa kama vichocheo vya majina ya utani lakini ilibainika kuwa majina haya hayafahamiki kwa wahusika. Data zinaonesha kuwa majina haya hutumika miongoni mwa wanafunzi pekee wanaolifahamu jina husika. Majina haya ya utani yanadhihirisha hali halisi ya walimu husika kitabia, kimaumbile na kimajukumu ni vigumu kuyatumia waziwazi. Data zinaonesha kuwa majina haya hayakupaswa kujulikana kwa hofu ya kuadhibiwa kwa utovu wa nidhamu dhidi ya walimu wao.

**Hitimisho**

Makala haya yamechunguza matumizi ya majina ya utani wanayopewa walimu wa sekondari nchini Tanzania. Mambo mbalimbali yamebainika katika utafiti huu ikiwa ni pamoja na vigezo vinavyotumika kutoa majina ya utani ya walimu. Vigezo vilivyotumiwa ni kama vile ufananisho wa wanyama, mada za masomo, vifupisho vya majina, uradidi wa maneno wakati wa uzungumzaji,ufananisho wa watu wengine, na mwonekano wa mavazi. Pia, makala haya yamebainisha kuwa majina ya utani yanachukua umaarufu mkubwa miongoni mwa wanafunzi na yana nafasi kubwa kimatumizi ukilinganisha na majina halisi ya wahusika ndani ya jamii na hususani katika muktadha wa shuleni. Vilevile, Mtafiti amebaini kuwa sio rahisi kwa mtu wa kawaida ambaye hayumo katika kundi la wanafunzi wa shule husika kujua maana au etimolojia ya jina ambalo mwalimu fulani kapewa. Data za utafiti zimedhihirisha kuwa majina ya utani yana maana zenye kurejelea uhalisi wa mwenye jina hilo.

**Marejeo**


Chevalier, S. (2004). Nicknames in Australia. *Bulletin Suisse de Linguistique Appliquée, 80* (Winter), 125-137.

Chevalier, S. (2006). *Ava to Zac: A sociolinguistic study of given names and nicknames in Australia.* Tubingen: Francke Verlag.

Crozier, W. R. (2002). Donkeys and Dragons: Recollections of schoolteachers' nicknames. *Educational Studies, 28*(2), 133-142.

Crozier, W. R., & Dimmock, P. S. (1999). Name-calling and nicknames in a sample of primary school children. *British Journal of Educational Psychology, 69*(4), 505-516.

de Klerk, V. na Bosch, B. (1996). Nicknames as sex-role stereotypes. *Sex Roles, 35*(9-10), 525-541.

Fernandez, C. (2008). Sociolinguistic patterns in onomastics. *Revista Española de Linguistica, 38*(2), 5-20.

Koss, G. (2006). Nicknames: Variation and internal differentiation in a linguistic field. *Beitrage zur Namenforschung, 41*(1), 1-12.

Mehrabian, A., and Piercy, M. (1993). Differences in positive and negative connotations of nicknames and given names. *The Journal of Social Psychology, 133,* 737-739.

Molefe, L. (2001). Onomastic aspects of Zulu nicknames with special reference to source and functionality. (Doctoral dissertation, University of South Africa, Pretoria, South Africa, 2000). *Dissertation Abstracts International, 62.*

Mutembei, A. K. (2009). UKIMWI Katika Fasihi ya Kiswahili. Taasisi ya Taaluma za Kiswahili, Chuo Kikuu Dar es Salaam. Tanzania.

Mshihiri, A.J. (1970). *Utani Relationships.* The Shambala. Dar es salaam: Chuo Kikuu cha Dar esSalaam (Haijachapishwa). Dar esSalaam, Tanzania.

Phillips, B. S. (1990). Nicknames and sex role stereotypes. Sex Roles 23(5): 281-289.

Sengo, T. S. Y., (2009). *Sengo na Fasihi za Kinchi.* Dar es Salaam: Al-amin Education and Research Academy.

Suta D.D., na Mnyamba, F.A. (1999). A Case of Reproduction and Articulation of Utani Among the Bena Ethnic Group in Tanzania.Dar es Salaam, Tanzania.

Starks, Donna and Kerry Taylor-Smith (2011). A Research Report on Nicknames and Adolescent Identity. *New Zealand Studies in Applied Linguistics* 17(2): 87–97.

Waziri, F. M.,& Dlourine, F. M. (1998). Makala "The Case of Reproduction and Articulation of Utani among the Pare in Tanzania". Dar es salaam, Tanzania.

Wilson, K.J. (2008). Icelandic nicknames. (Doctoral dissertation, University of California, 2007). *Dissertation Abstracts International.*

Wong, S. Y. J. (2007). Nicknames in Hong Kong and England: Forms, functions and their relation to personal names and other forms of address (Doctoral dissertation, Open University, Milton Keynes, United Kingdom, 2007). *Dissertation Abstracts International.*